

LAIKIPIA



UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

**1<sup>ST</sup> SEMESTER 2025/2026 ACADEMIC YEAR**

### **EXAMINATIONS FOR MASTERS OF ARTS KISWAHILI NA MAWASILIANO**

**KICO 825: MBINU ZA UHARIRI KATIKA KISWAHILI**

***STREAM: R***

***TIME: 3 HRS***

***DAY: WEDNESDAY (8.30-11.30AM)***

***DATE: 04/02/2026***

**THIS QUESTION PAPER CONSISTS OF THREE (3 PAGES)**

**PLEASE DO NOT OPEN UNTIL THE INVIGILATOR SAYS SO.**

**MAAGIZO**

Jibu maswali **matatu**.

Swali la **kwanza** ni la lazima.

**SWALI LA KWANZA**

- (a) Hariri matini hii kwa kutumikisha ishara za kihariri / usomaji wa kisarifu. **(alama 20)**

Katika hadithi shongake dada ana ndveu Bwana masudi na mkewe Bi Hamida wanamwamini na kufmurahia sana binti yao Safia kulingana ambaye nao si mtovu wa maadili kama watoto wengine waliokuwa katika eneo hilo Yakini majirani na wakzi wingine wa eneo hilo walimsifia Safia kwa uzuri na nidamu yake. She is a good girl hana tabia za wendaguu kama alizo nazo Mkadi ndivyo walivyo semwa Bada ya kitbo kidogo safia anaomba rafiki yake Kimwana aruhusiwe kuja kusoma kwao naye

Siku moja wakila chakula cha mchana, Lulua anawaeleza kuhusu alivyo wakuta Safia na shongake wakiwa wamelala kitandani. Alitaja shonganke Safia aliuwa na ndevu. ni wakati huu wa simulizi za Lulua Bw. masundi anapopigiwa simu ya kumwarifu kuwa Safia amekufwa akinjarimbu kuafya miba. Akikua katika hospitali ya vuamimba.

- (b) Kwa mifano mwafaka, tathmini nafasi ya alama za uakifishaji kama nyenzo ya uhariri wa magazeti. **(alama 10)**

**SWALI LA PILI**

- a) Tofautisha uhariri na usarifu matini? **(alama 3)**
- b) Eleza hali sita zinazoweza kumlazimu mhariri wa habari kubuni msamiati na kwa mifano ueleze mbinu atakazotumia kubuni msamiati huo. **(alama 12)**

**SWALI LA TATU**

- a) Kuna maadili na kanuni zinazoongoza uhariri kama sehemu ya mawasiliano. Eleza. **(alama 10)**
- b) Eleza umuhimu na nafasi ya uhariri wa makala katika vyombo vya habari. **(alama 5)**

**SWALI LA NNE**

‘Uhariri ndio uti wa mgongo wa shirika lolote’. Jadili.

**(alama 15)**

**SWALI LA TANO**

Eleza majukumu yanayotekelezwa na mhariri wa gazeti katika mashirika ya uchapishaji wa magazeti.

**(alama 15)**